# Maswali Yanayoulizwa Sana Kuhusu Kuweka Oda Mtandaoni

**Swali:** Je, ni maduka gani ya kuuza bidhaa za vyakula na matumizi ya nyumbani yanatoa huduma za manunuzi ya mtandaoni kwa WIC?

**Jibu:** Kwa sasa, ni maduka ya Walmart ya Washington pekee yanayotoa huduma za manunuzi ya mtandaoni kwa WIC.

**Swali:** Je, hii inajumuisha Walmart Neighborhood Markets na Walmart Supercenters?

**Jibu:** Maeneo yote ya Walmart yaliyopo Washington yameidhinishwa na WIC.

**Swali:** Je, hii inajumuisha maduka ya Walmart yanayopatikana kati ya jimbo moja na jimbo jingine au katika miji ya mipakani?

**Jibu:** Kuna duka moja la Walmart katika mji wa mpakani lililoidhinishwa ambalo halipo katika jimbo la WA (Warrenton, OR).

**Swali:** Je, familia za WIC zinahitaji kuwa na wasifu wa Walmart iili kuweza kufanya manunuzi mtandaoni?

**Jibu:** Ndiyo, hatua ya kwanza ya kufanya manunuzi mtandaoni ni kuunda wasifu wa kufanya manunuzi. Hakuna gharama inayohusiana na kuandaa wasifu.

**Swali:** Je, ninawezaje kupakua programu ya Walmart?

**Jibu:** Tumia mojawapo ya viungo hapo chini ili kupakua programu ya Walmart.

- Apple Store: Programu za Walmart kwenye App Store (kwa Kiingereza; baadhi ya lugha za ziada zinapatikana)
- Google Play: Walmart Manunuzi na Kuokoa Fedha - Programu kwenye Google Play (kwa Kiingereza)

**Swali:** Je, nitajuaje ni vyakula gani vinavyostahiki WIC katika Walmart?

**Jibu:** Kwenye Walmart.com (kwa Kiingereza) au kwa programu yako ya Walmart unaweza kutumia upau wa kutafuta ili kutafuta vyakula vyako vya WIC. Kwa mfano, ikiwa unatafuta maziwa yaliyoidhinishwa na WIC, unaweza kuandika “WIC Milk (Maziwa ya WIC)” kwenye upau wa kutafuta. Vyakula vinavyostahiki WIC vitaonyesha lebo ya “**WIC Eligible (Inastahiki WIC)**”. Pia unaweza kununua vyakula vilivyoidhinishwa na WIC pekee kwa kutumia Shop your **WIC benefits (Nununua manufaa yako ya WIC)**, ambapo kwa sasa inayo orodha ya vyakula vyako vya WIC.

**Swali:** Je, bado ninaweza kuendelea kufanya manunuzi mtandaoni ikiwa nitabadilisha kadi yangu ya WIC?

**Jibu:** Ndiyo, unaweza kufuta kadi yako ya zamani ya WIC kwenye wasifu wako wa Walmart kisha ukaweka nambari za kadi yako mpya.

**Swali:** Je, ninawezaje kufanya malipo kwa kutumia kadi yangu ya WIC wakati wa kufanya manunuzi mtandaoni katika Walmart?

**Jibu:** Ingia kwenye akaunti yako ya Walmart (mtandaoni kwenyeWalmart.com (kwa Kiingereza) au kwenye programu ya Walmart) na bofya “Add new payment method **(Ongeza njia mpya ya malipo)**” au “**Add payment card (Ongeza kadi ya malipo)**. Weka nambari ya kadi yako ya WIC na PIN ya WIC. Unapofanya malipo, tovuti itakuomba uweke PIN yako ya WIC tena.

# Maswali Yanayoulizwa Sana Kuhusu Kuweka Oda Mtandaoni

**Swali:** Je, ninaweza kununua vyakula vya WIC na vyakula visivyo vya WIC kwa pamoja?

**Jibu:** Ndiyo, unaweza kutumia kadi yako ya WIC kwa vyakula vya WIC ulivyochagua kisha ukatumia njia nyingine ya malipo kwa vyakula vyako visivyo vya WIC au bidhaa nyingine.

**Swali:** Je, ninalipia ada ya kuletewa/kusafirisha pale ninaponunua bidhaa za WIC?

**Jibu:** Ndiyo, utapaswa kulipia ada ya kuletewa ikiwa utachagua chaguo la kuletewa. WIC haigharimii ada za kuletewa/kusafirisha. Ikiwa wewe ni mwanachama wa Wal-Mart + kuletewa/kusafirisha ni bure. Hakuna ada kwa kuchukua mwenyewe bidhaa za vyakula na matumizi ya nyumbani. Si anwani zote za WA zinastahiki huduma ya kuletewa.

**Swali:** Je, nini kitatokea ikiwa nitakosea kuweka PIN yangu na tovuti ikanizuia kuingia kwenye Walmart.com?

**Jibu:** Baada ya kuweka PIN isiyo sahihi mara nne, Walmart.com itafunga akaunti hadi saa sita usiku za siku hiyo. Ikiwa ungependa kuweka upya PIN yako, piga simu kwenye namba iliyopo nyuma ya kadi yako ya WIC.

**Swali:** Je, orodha yangu ya manufaa itasasishwa mara tu nitakapoweka oda yangu?

**Jibu:** Ndiyo, salio la manufaa yako yaliyopo litasasishwa mara tu utakapoweka oda yako.

**Swali:** Je, familia za WIC zinaweza kubadilishana/kubadilisha vyakula vilivyoidhinishwa kwa WIC?

**Jibu:** Ndiyo, familia za WIC zinaweza "Start a Return (Kuanzisha Urejeshaji)" kwenye mtandao ili kubadilishana kwa bidhaa sawa na hiyo iliyoidhinishwa na WIC. Pia zinaweza kwenda kwenye dawati la huduma kwa wateja kwenye Walmart ili kuanzisha ubadilishanaji. Kubadilishana bidhaa karibu na siku ya mwisho ya kipindi cha manufaa yako kunaweza kusababisha ukosefu wa muda wa kutosha kwa ajili ya uchakataji.

**Swali:** Je, familia za WIC zinaweza kurejeshewa fedha pale ambapo bidhaa hazipatikani wakati wa utekelezaji?

**Jibu:** Ndiyo, Familia za WIC zinawza kuchagua bidhaa mbadala wakati zikiwa zinafanya manunuzi mtandaoni. Ikiwa bidhaa iliyochaguliwa haipo na bidhaa mbadala haikuchaguliwa, bidhaa ambazo hazipo zitarejeshwa kwenye akaunti ya manufaa ya mshirika kwa ajili ya kununuliwa wakati mwingine.

**Swali:** Je, nitatozwa ada ya mfuko?

**Jibu:** Hapana, hutatozwa ada za mifuko wakati unapoweka oda mtandaoni ukitumia kadi ya WIC.

**Swali:** Je, ni maduka gani ya Walmart yanayoruhusu kuchukua bidhaa pembezoni mwa barabara?

**Jibu:** Maduka yote ya Walmart katika jimbo la Washington yameidhinishwa na WIC na yanatoa huduma ya kuchukua bidhaa pembezoni mwa barabara.

**Swali:** Je, kuna kiwango cha chini cha oda ya kuagiza mtandaoni?

**Jibu:** Hapana, hakuna kiwango cha chini cha oda.

# Maswali Yanayoulizwa Sana Kuhusu Kuweka Oda Mtandaoni

**Swali:** Je, kuna kiwango cha chini cha oda ya kusafirishwa bila malipo?

**Jibu:** Hapana, gharama za usafirishaji zinaweza kutumika. Washiriki wa WIC wanastahiki kupata usajili wa Walmart + wenye punguzo ambao unahusisha usafirishaji bila malipo na bila kiwango cha chini cha oda.

**Swali:** Je, ni siku gani ya mwisho ambayo ninaweza kuweka oda mtandaoni kwa ajili ya kuchukua bidhaa pembezoni mwa barabara au kuletewa?

**Jibu:** Unapaswa kuchukua oda yako ndani ya kipindi chako cha manufaa. Tunapendekeza ufanye manunuzi kabla ya siku ya mwisho ya manufaa yako.

**Swali:** Je, Walmart inaweza kutoa mbadala wa chakula cha WIC ikiwa bidhaa imekwisha?

**Jibu:** Ndiyo, lakini ikiwa tu ulichagua bidhaa mbadala unayoipendelea kwa kila bidhaa wakati wa oda yako ya mwanzo. Unapokagua oda yako wakati wa kufanya malipo, utapatiwa chaguo la kuchagua mbadala.

**Swali:** Je, niwasiliane na nani ikiwa kuna tatizo linalohusiana na oda ya mtandaoni ya WIC?

**Jibu:** Unaweza kupiga simu kwa 1(800)-925-6278 au tembelea Usaidizi - Walmart.com (kwa Kiingereza).

**Swali:** Je, ninaweza kutumia zaidi ya Kadi moja ya WIC ikiwa nina kadi nyingi kwenye familia yangu?

**Jibu:** Hapana, huwezi kutumia zaidi ya Kadi moja ya WIC kwa muamala ule ule wa oda ya mtandaoni kwa sababu ni aina moja ya kadi. Unaweza kutumia aina nyingine ya malipo kama vile Supplemental Nutrition Assistance Program (SNAP, Programu ya Msaada wa Chakula cha Ziada), Electronic Benefit Transfer (EBT, Uhamisho wa Mafao Kielektroniki), kadi ya benki, kadi ya mkopo, n.k. Utahitajika kuweka oda tofauti mtandaoni kwa kila Kadi tofauti ya WIC.

Washington State Department of HEALTH

DOH **961-1319** February 2025 Swahili

Ili kuomba hati hii katika muundo mwinginee, piga simu kwa 1-800-841-1410.

Kwa watu walio na ulemavu au matatizo ya kusikia, tafadhali piga simu kwa 711 (Washington Relay) au tuma barua pepe WIC@doh.wa.gov.